HOTUBA YA NAIBU KATIBU MKUU ANDERSON MUTATEBWA, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU) WAKATI WA UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA KUIMARISHA UWEZO WA KUZUIA NA KUJIANDAA KUKABILIANA NA MADHARA YA EL NINO KWA KAMATI YA USIMAMIZI WA MAAFA MKOA WA PWANI, TAREHE 27 SEPTEMBER, 2023

- **Mhe. Abubakari Mussa Kunenge, Mkuu wa Mkoa wa Pwani;**
- **Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya mliopo;**
- **Waheshimiwa Wenyekiti wa Halmashauri mliopo;**
- **Katibu Tawala wa Mkoa;**
- **Wakurugenzi wa Halmashauri mliopo;**
- **Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini – OWM-SBU;**
- **Wataalamu kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani,**
- **Waratibu wa Maafa kutoka Halmashauri za Manispaa,**
- **Wawezeshaji kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Polisi Tanzania na DarMAERT;**
- **Wawakilishi wa Taasisi mbalimbali;**
- **Viongozi wa Dini;**
- **Waandishi wa habari;**
- **Mabibi na Mabwana;**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…

Ndugu Washiriki;

Awali ya yote naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kufika siku hii ya leo tukiwa salama. Aidha, napenda kuwashukuru wote kwa kuitikia wito wa kufika kushiriki kikao kazi cha utekelezaji wa hatua za kuzuia na kupunguza madhara pamoja na kuimarisha uwezo wa kukabiliana na maafa yanayoweza kusababishwa na uwepo wa El Nino.

Ndugu Washiriki,

Kikao kazi cha leo kimezingatia wajibu mlio nao kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Namba 6 ya Mwaka 2022 na Kanuni zake, ambayo imeanzisha Kamati za Usimamizi wa Maafa za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji au Mitaa. Jukumu la msingi la Kamati hizi ni kuchukua hatua kwa lengo la kuzuia na kupunguza madhara ya majanga ya aina zote na kujiandaa kukabili na kurejesha hali kwa ubora zaidi endapo maafa yatatokea.

Ndugu Washiriki,

Sote tunatambua kuwa matukio ya maafa yanatokea na kusababisha madhara katika ngazi ya jamii ambapo Serikali za Mitaa, kuanzia Kitongoji, Mtaa au Kijiji na Jiji, Manispaa, Mji na Wilaya zinawajibika moja kwa moja. Hatua za kuzuia madhara zinatekelezwa zaidi na viongozi na wataalam kwa kushirikiana na wadau na wananchi katika maeneo haya. Tumekutana leo kukumbushana wajibu muhimu mlio nao kwa kila mmoja kuwajibika katika eneo lake ili kuokoa maisha na kulinda mali za wananchi. Tukumbuke kuwa Mkoa unaingia kusaidia juhudi za halmashauri husika pamoja na kushirikisha uratibu wa msaada kutoka ngazi ya taifa endapo madhara yatakuwa yamezidi uwezo wa rasilimali katika eneo husika.

Ndugu Washiriki,

Napenda kusisitiza kila mmoja kuchukua hatua katika eneo lake, ikumbukwe kuwa mfumo wa Serikali umezingatia wajibu wa sekta na taasisi yenye jukumu kisera na kisheria kuchukua hatua ili kuokoa maisha na mali za jamii yetu kutokana na matukio ya maafa. Uzoefu unaonesha kuwa kuchukua hatua za mapema za kuzuia na kupunguza madhara

zimekuwa na gharama nafuu kuliko kusubiri ili kuchukua hatua baada ya maafa kutokea ambapo, Serikali imekuwa ikilazimika kutumia fedha nyingi.

Ndugu Washiriki,

Hata hivyo, endapo hatua za kuzuia madhara zitashindikana, tukumbuke kuwa hatua za kukabiliana na maafa wakati wa tukio zinatekelezwa na taasisi zinazotoa *huduma za msingi* katika eneo la tukio husika ili kuokoa maisha na mali. Nisisitize taasisi zinazohusika mstari wa mbele wakati wa tukio la maafa zinapaswa kujiandaa kikamilifu kwa kuweka utaratibu wa pamoja ikiwa ni pamoja na kuwa na mpango wa dharura wa utendaji na utaratibu wa mawasiliano wakati wa dharura ili ziweze kuchukua hatua kwa haraka na ufanisi ili kuokoa maisha. Taasisi hizo ni pamoja na zile zinazohusika na huduma ya utafutaji na maokozi, usalama wa wananchi, afya na makazi ya muda na huduma zingine za kijamii. Aidha, taasisi zinazohusika kutoa huduma wezeshi au saidizi pamoja na kuimarisha mifumo kama vile usafiri, mawasiliano, nishati na maji zinakumbushwa kujiimarisha ili kuhakikisha shughuli za kijamii na kiuchumi haziathiriki wakati wa maafa. Taasisi saidizi zina wajibu wa kuwezesha taasisi zenye jukumu ongozi katika kuokoa maisha na mali ili zitekeleze majukumu kwa ufanisi pamoja na kupunguza athari kwa jamii.

Ndugu Washiriki,

Kazi tunayoifanya leo ni mwendelezo wa hatua ambazo Serikali inaendelea kuchukua katika kuzuia madhara kufuatia utabiri wa mwelekeo wa mvua za msimu wa Vuli kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba 2023 kuonesha uwepo wa El-Niño itakayosababisha vipindi vya mvua kubwa kwa mwezi Oktoba mpaka Disemba 2023 na kuendelea mpaka Mwezi Januari 2024. Historia inaonesha madhara yanayoweza kutokea katika sekta kutokana na uwepo wa El Nino utakaosababisha mvua kubwa ni pamoja na:-

(a) Mafuriko kuharibu miundombinu mbalimbali, madhara ya kiafya, kiuchumi, kijamii na upotevu wa mali.

(b) Maporomoko ya ardhi kuathiri makazi, mazingira, mashamba, usafiri na shughuli zingine hususani uchimbaji madini.

(c) Magonjwa ya milipuko kwa binadamu na wanyama na wadudu waharibifu wa mazao na mimea.

Ndugu Washiriki,

Serikali ilianza kutekeleza hatua za kuzuia madhara haya toka mwezi Julai 2023 wakati taarifa ya awali ya dalili za uwezekano wa uwepo wa El Nino ilipotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania. Hivyo, tukio linalofanyika leo hii hapa Manyara ni mwendelezo wa hatua hizo na linahusisha mikoa mingine 14. Uzinduzi ninaofanya leo unahusisha kazi zitakazoendelea katika mikoa hiyo mpaka tarehe 30 Septemba, 2023. Mikoa hiyo ni ile inayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ambayo ni Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, kusini mwa mkoa wa Simiyu, kaskazini mwa mkoa wa Kigoma, Dar es Salaam, Tanga, Pwani (ikiwemo visiwa vya Mafia) na kaskazini mwa mkoa wa Morogoro. Kazi hii imezingatia uwajibikaji wa pamoja ambapo, Ofisi ya Waziri Mkuu imeshirikiana na Wizara za kisekta na Taasisi za Serikali na Wadau kuendelea kuimarisha hatua ambazo zinaendelea kuchukuliwa na Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa katika Mikoa husika.

Ndugu Washiriki,

Naomba nirejee maelekezo mahsusi yaliyotolewa na Serikali awali kwa Mikoa na Wilaya kupitia Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi zote, ili kuchukua hatua dhidi ya uwepo wa hali ya El Nino ili kuzuia na kupunguza madhara pamoja na kujiandaa kukabili na kurejesha hali. Hatua zilizoelekezwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuainisha na kuandaa rasilimali za kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na maafa endapo yatatokea kwa kila sekta kushiriki kikamilifu katika eneo lake.

(b) Kutambua maeneo hatarishi yenye viashiria vya kuathirika na maafa na kuandaa mipango ya kuzuia madhara na kukabiliana na maafa endapo yatatokea.

(c) Wananchi wahimizwe kuhama kwenye maeneo hatarishi na kutekeleza shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo salama.

(d) Kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuweka akiba ya chakula na kulima mazao yanayotumia maji mengi.

(e) Kuelimisha wananchi juu ya hatua za kuchukua tahadhari ili kuokoa maisha na mali.

(f) Kuandaa na kutekeleza mipango ya kuzuia milipuko ya magonjwa kwa binadamu, wanyama na mimea.

(g) Idara na taasisi zinazohusika na mazingira na miundombinu, zihakikishe barabara zinapitika wakati wote, mitaro na makalvati yanaimarishwa na kusafishwa.

(h) Sekta za maji, umeme na mawasiliano ziweke mipango kuzuia madhara na kuhakikisha uharibifu katika huduma hizo unapewa ufumbuzi mapema.

(i) Kushirikisha wadau wa maafa (Wananchi, Taasisi na Sekta binafsi) katika mipango yote ya usimamizi wa maafa.

(j) Kutoa taarifa haraka kwa mamlaka husika inapotokea maafa katika maeneo yenu.

(k) Kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya maokozi na huduma za dharura kwa kuzingatia historia ya El Nino na hali ya sasa katika maeneo yenu.

(l) Kutoa elimu kwa watendaji katika ngazi zote ili wachukue hatua stahiki kuzuia na kupunguza madhara ya El Nino yanayoweza kutokea.

(m) Kuimarisha na kusafisha njia za maji ya mvua na maji taka pamoja na usimamizi wa taka ngumu na uwepo wa madampo.

(n) Kuimarisha madaraja na kingo za Mito na Mabwawa katika maeneo yote ya kimkakati nchini.

(o) Kusimamia matumizi sahihi ya mitaro na njia za maji kwa kuzuia viwanda kutiririsha uchafu katika maeneo ya makazi na sehemu za uzalishaii mali.

(p) Mikoa na halmashauri iandae mipango ya utekelezaji katika maeneo yao kwa kuzingatia Mpango wa Taifa wa Dharura wa Kukabiliana na Madhara ya El Nino.

(q) Kuhakikisha mvua hizi zinatumika kwa shughuli za maendeleo ikiwemo kilimo, uandaaji wa mabwawa na malambo kwa ajili ya kuvuna maji, uzalishaji wa samaki na kuandaa malisho kwa ajili ya mifugo.

(r) Kufuatilia na kutekeleza maelekezo ya kitaalam pamoja na taarifa za utabiri wa hali ya hewa unaotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wa kila siku, siku 5, siku 10 na wa siku 30 ili kuchukua hatua stahiki.

Ndugu Washiriki;

Tunapongeza mikoa na halmashauri kwa kuchukua hatua za mapema kutekeleza maelekezo haya. Ofisi ya Waziri Mkuu imepokea taarifa na mipango iliyowasilishwa na sekta ikiwemo miundombinu, kilimo, maji, uchukuzi, nishati na nyinginezo kuhusu namna ambavyo wanachukua hatua katika maeneo yao. Nawapongeza kwa hatua mnazochukua na leo nitashiriki kukagua baadhi ya maeneo kuona utekelezaji katika maeneo husika. Nitashiriki kutembelea baadhi ya maeneo korofi kwa mafuriko na kuona hatua ambazo zinaendelea kuchukuliwa katika kuzuia na kupunguza madhara yanayoweza kusababisha na mvua za El Ninona.

Ndugu Washiriki;

Ni jukumu lenu kila mmoja katika nafasi yake kama mjumbe wa Kamati za Usimamizi wa Maafa kutekeleza kimamilifu hatua za kuchukua katika sekta zenu kwa kuzingatia kuwa madhara yanaweza kuongezeka endapo hatua stahiki hazitachukuliwa kwa wakati. Natarajia kuwa baada ya kikao kazi cha leo, Kamati hasa ngazi ya Halmashauri zote za Mkoa zitaimarisha

utekelezaji wa hatua za kuzuia madhara ili kuhakikisha tunaokoa maisha na mali kwa ustahimilivu wa taifa.

Hatua hii ni muhimu ili kuhakikisha juhudi zinazochukuliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuimarisha uchumi na huduma za kijamii katika ujenzi wa Taifa letu zinakuwa stahimilivu dhidi ya maafa. Ni dhahiri kuwa hatua mnazochukua zitachangia katika juhudi zake katika kuongoza na kusimamia utekelezaji wa mipango ya Serikali pamoja na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025 kwa manufaa makubwa kwa wananchi na tija iliyokusudiwa.

HITIMISHO

Usimamizi wa maafa ni jukumu letu sote, kila mmoja ashiriki sasa na kuchukua hatua katika eneo lake ili kuokoa na kulinda maisha, mali na mazingira.

Baada ya kusema maneno haya, naomba kutamka kuwa kikao kazi cha kuimarisha uwezo wa kukabiliana na madhara ya El Nino kwa Kamati ya Usimamizi wa Maafa Mkoa wa Pwani kimefunguliwa rasmi.

Asanteni kwa kunisikiliza, na nawatakia mafunzo mema!!!

KATIBU MKUU